

Maswali

1. Tauni ya kwanza ilikuwa nini?
2. Tauni ya pili ilikuwa nini?
3. Tauni ya tatu ilikuwa nini?
4. Tauni ya nne ilikuwa nini?
5. Tauni ya tano ilikuwa nini?
6. Tauni ya sita ilikuwa nini?
7. Tauni ya saba ilikuwa nini?
8. Tauni ya nane ilikuwa nini?
9. Tauni ya tisa ilikuwa nini?
10. Tauni ya kumi ilikuwa nini?

Majibu

1. Tauni ya kwanza mito ilikuwa damu
2. Tauni ya pili ilikuwa vyura
3. Tauni ya tatu ilikuwa chawa
4. Tauni ya nne ilikuwa inzi
5. Tauni ya tano ilikuwa ugonjwa wa mifugo
6. Tauni ya sita ilikuwa majibu ya kufura (uvimbe)
7. Tauni ya saba ilikuwa mvua ya mawe
8. Tauni ya nane ilikuwa nzige
9. Tauni ya tisa kulikuwa na giza
10. Tauni ya kumi ilikuwa kufa kwa wazaliwa wa kwanza.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM




Awamu ya 1 Mwaka wa 1

16 Tauni katika Misri

Marejeo

Kutoka: 5-12



Kiini cha somo

Kuonyesha hukumu mbaya kwa hao wanaoasi Mungu.

Maneno maalum

1. Musa aenda Misri +akutana na Haruni + wanaonana na Farao + watu wanafanya kazi zaidi
2. Musa apiga maji + mto ukawa damu + vyura
3. Chawa + inzi + ugonjwa wa mifugo + majibu ya kufura (uvimbe) + moyo wa Farao mugumu
4. Mvua ya mawe + nzige + giza + watu hawakuenda.
5. Tauni ya mwisho + usiku wa manane + wazaliwa wa kwanza + Farao awaambia waende + wana wa Israeli watoke Misri


16.1 Musa alirudi Misri kwa ajili Mungu alimwambia. Njiani alikutana na kakake Haruni. Wote wawili walienda kuona Farao.

“Mungu amesema, ‘Waache watu wangu waende,’” Musa alimwambia Farao. “Bwana ni nani?” Farao alisema, “Eti ni mtii? Sitawaacha Waisraeli waende Mtawafanya watu wasifanye kazi.”

Kwa hivyo Farao aliwaambia wanyapara wawafanye wana wa Israeli wafanye kazi nyingi zaidi.

16.2 Musa alienda kwa Farao tena. “Nitapiga maji ya mto na fimbo iliyo mkononi mwangu, yatageuka yawe damu. Halafu utajua Bwana ni nani,” akasema Musa, alinua fimbo na kupiga maji ya mto na yakageuka kuwa damu. Watu hawangeweza kuyanywa na samaki wakakufa wote.

“Bwana asema, ‘Waache watu wangu waende’” Musa alimwambia Farao. “Usipowaachilia waende vyura watatoka mtoni na kuingia kwa nyumba zenu, kwa vyumba vya kulala na hata kwa meko yako.” Musa akanyosha mkono kwa mto na vyura wote wakatoka na kufunika nchi ya Misri.




Farao akaita Musa. “Ambia Bwana atoe hawa vyura,” Farao akasema, “nitawaacha watu waende.” Lakini alibadilisha mawazo yake. Alifanya moyo wake kuwa mugumu kwa kutowaachilia.



16.3 Kwa hivyo Mungu akawatumia chawa (wadudu wadogo kama viroboto) juu ya nchi na kukawa na chawa kwa watu na wanyama. Lakini Farao hakuwaachilia watu waende.

Mungu akawawekea uvimbe kwa watu na wanyama. Lakini moyo wa Farao ulikuwa mugumu hakuwaacha waende.

16.4 Mungu akawatumia mvua ya mawe ikauwa wanyama na watu waliokuwa nje. Lakini Farao hakutaka kuwaacha watu waende.



“Mpaka lini utakataa kutii Bwana?” Musa aliuliza. Kwa hivyo Mungu alileta tauni ya nzige ikakula kila mmea wa shamba. Baada ya hii akaleta giza kuu kwa nchi ya Misri, lakini Farao hakutii Bwana awaachilie watu waende.

16.5 Mungu akasema, “Nitatuma tauni ingine moja Misri. Usiku wa manane, wazaliwa wa kwanza wa wanyama na wa watu wote watakufa. Na Farao atamuacha muende.”

Usiku wa manane Mungu alituma malaika kuuwa wazaliwa wa kwanza nchini Misri, kutoka kwa wa Farao mpaka kwa wa wajakazi. Kulikuwa na kilio kikuu nchini kwa sababu wazaliwa wa kwanza wote walikufa.

Farao akaita Musa. “Enda” Farao alisema, “mkamtumikie Bwana. Chukua kila kitu chenu.” Kwa hivyo wana wa Israeli walitoka Misri kuelekea nchi ya ahadi.